**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**

**(EWURA)**

**MALALAMIKO NAMBA. GA.71/472/NZ/2024/06**

**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000151**

**KATI YA**

**DANIEL MESHACK SAMBAI ............................................................**

**MLALAMIKAJI**

**NA**

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA**

**ARUSHA (AUWSA) ............................................................................**

**MLALAMIKIWA**

---

# TUZO YA MAKUBALIANO

---

***(Imetolewa na Kamati ya Sheria na Utawala ya Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA katika kikao chake cha 146 cha tarehe 17 mwezi Machi 2025)***

## 1. Maelezo ya Awali

Mnamo tarehe 19 Juni 2024, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa Bw. Daniel Meshack Sambai akiwakilishwa na Bi. Endesh Daniel Sambai, wa Mita 200 Ngarenaro Wilaya ya Arusha Jijini Arusha, ("Mlalamikaji") dhidi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA) ("Mlalamikiwa"). Mlalamikaji anamtaka Mlalamikiwa kufanya uchunguzi wa ankara kubwa ya majitaka na kufuta deni la kiasi cha Shilingi 8,263,539/= la maji taka katika akaunti yake namba A16404795901 yenye dira namba 04795901 ambayo ina jina la Daniel M. Sambai deni ambalo halitambui.

Mlalamikaji anaeleza kwamba hakumbuki kujiunga na huduma ya majitaka pekee katika nyumba zake alizoziorodhesha katika barua alizomwandikia Mlalamikiwa, na hakuna ushahidi wowote unaojitosheleza wa kuweza kubainisha matumizi hayo ya gharama ya kiasi cha Shilingi 130,000/= kwa mwezi kama gharama ya majitaka ambayo imefikisha deni la Shilingi 10,227,039/= hadi kufikia sasa.

Mlalamikaji aliwasilisha malalamiko yake ofisini kwa Mlalamikiwa lakini hakupata ufumbuzi, ndipo alipoamua kuwasilisha Malalamiko yake kwa Mamlaka (EWURA) Kanda ya Kaskazini na kuiomba Mamlaka kumuamuru Mlalamikiwa kufuta deni hilo la majitaka ambalo halifahamu na halina uhalali.

Baada ya kupokea malalamiko, tarehe 25 mwezi Juni 2024, Mamlaka (EWURA), ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni za EWURA za Utatuzi wa Migogoro, TS Na. 428/2020 - (EWURA (*Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules* 2020)).

Mlalamikiwa aliwasilisha utetezi wake tarehe 23 mwezi Agosti 2024, na kuieleza Mamlaka kwamba, Mlalamikaji ni mteja wa huduma ya majitaka na majisafi, na kwamba akanunti namba A16404795901 yenye dira namba 04795901 (AC-AC) ilifunguliwa mwaka 2017 kwa ajili ya majitaka tu, na ni kwa mteja anayetumia huduma ya majitaka pekee. Na kwamba hapo awali wateja wa aina hii walikua wanatozwa gharama kwa utaratibu wa makadirio (*flat rate*) kutegemea na ukubwa wa biashara.

Mlalamikiwa anaeleza zaidi kwamba, Mlalamikaji analitambua deni bishaniwa kwani hapo nyuma aliwahi kufika ofisini kwa Mlalamikiwa na kuweka utaratibu wa kulipa deni hilo na kuahidi kurudi baada ya kufanya malipo ya awamu ya kwanza lakini hakurudi tena.

Kikao cha usuluhishi kati ya Wadaawa kilifanyika tarehe 22 na 23 mwezi Januari 2025, katika ukumbi wa mikutano wa ofisi za EWURA Kanda ya Kaskazini Jijini Arusha. Mwisho wa kikao cha usuluhishi, pande zote mbili zilikubaliana kwamba:

**(a)** Mlalamikiwa atafuta deni la kiasi cha shilingi 6,033,500/= kutoka deni la Shilingi 11,024,539 kwenye akaunti namba A16404795901 yenye jina la Daniel M Sambai kufikia tarehe 23 mwezi Februari 2025.

**(b)** Mlalamikiwa atahamisha deni la kiasi cha Shilingi 2,575,518.54 kutoka katika akaunti namba A16404795901 yenye jina la Daniel M Sambai kwenda akaunti namba A16400736301 yenye jina la Daniel M. Sambai kufikia tarehe 23 mwezi Februari 2025.

**(c)** Mlalamikaji atalipa deni la kiasi cha Shilingi 4,991,039 kwa awamu kupitia akaunti namba A16404795901 yenye jina la Daniel M Sambai kama ifuatavyo:

(a) Kiasi cha Shilingi 1,247,759.75 kitalipwa kufikia tarehe 28 mwezi Februari 2025; na

(b) Kiasi kinachobaki cha Shilingi 3,743,279.25 kitalipwa ndani ya miezi 12 kuanzia mwezi Machi 2025.

Makubaliano haya yamefupishwa kimaandishi kama inavyoainishwa kwenye Kanuni ya 14 (4) ya Taratibu za Utatuzi wa Migogoro na kama inavyoainishwa kwenye fomu ya makubaliano.

## 2.0 Makubaliano

Pande zote mbili zimefikia muafaka kwamba;

**(a)** Mlalamikiwa atafuta deni la kiasi cha Shilingi 6,033,500/= kutoka deni la Shilingi 11,024,539 kwenye akaunti namba A16404795901 yenye jina la Daniel M Sambai kufikia tarehe 23 mwezi Februari 2025;

**(b)** Mlalamikiwa atahamisha deni la kiasi cha Shilingi 2,575,518.54 kutoka katika akaunti namba A16404795901 yenye jina la Daniel M. Sambai kwenda akaunti namba A16400736301 yenye jina la Daniel M. Sambai kufikia tarehe 23 mwezi Februari 2025; na

**(c)** Mlalamikaji atalipa deni la kiasi cha Shilingi 4,991,039 kwa awamu kupitia akaunti namba A16404795901 yenye jina la Daniel M Sambai kama ifuatavyo

(a) Kiasi cha Shilingi 1,247,759.75 kitalipwa kufikia tarehe 28 mwezi Februari 2025; na

(b) Kiasi kinachobaki cha Shilingi 3,743,279.25 kitalipwa ndani ya miezi 12 kuanzia mwezi Machi 2025.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 14 (5) ya Taratibu za Utatuzi wa Migogoro makubaliano haya yameandikishwa kama Tuzo ya Mamlaka. Kila pande itabeba gharama zake katika shauri hili.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 17 mwezi Machi 2025.

..............................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**